

HALUSINESHENI, DELUSHENI NA UGONJWA WA PARKINSON



Kuna watu walio na ugonjwa wa Parkinson ambao hukumbwa na halusinesheni na delusheni, dalili ambazo hutokea sana sana hali ya mgonjwa inapozorota. Halusinesheni ni hali ya kuona, kusikia au kuhisi vitu visivyokuwepo. Delusheni ni fikira, imani au wasiwasi wenyewe msingi usiyo wa ukweli lakini huonekana kuwa ukweli kwa mgonjwa. Maluweluwe ni hali ya kuwa na fikira zisizo sahihi kuhusu jambo fulani, kwa mfano, huenda ukadhani pazia ni kikundi cha watu. Mambo kama haya yanaweza kuwa ya kutia wasiwasi kwa mgonjwa wa Parkinson na kwa familia yake, lakini ni muhimu kufahamu kuwa dalili hizi ni za kawaida na hutokana na dawa za PD, magonjwa ya kuambukizwa au wakati mwingine mwanzo wa demenshia.

AINA ZA HALUSINESHENI



Halusinesheni maono au njozi bila kuwa na kichocheo cha nje ya kiungo cha fahamu kinachohusika. Halusinesheni hutokea kama hisia za kusikika, kunuswa au kuonjwa, na huenda zikawa madhara ya madawa:

- **halusinesheni za kuona** hutokea kwa rangi nyeusi na nyeupe ama rangi tofauti tofauti, huenda zikatokea kama picha au kama ndoto (ilhali hujalala). Huenda zikahusu wanyama wadogo au watoto na huenda zikaonekana kwa muda mrefu au zikapotea haraka. Halusinesheni hizi hutokea sanasana katika wakati wa mwangaza mdogo
- **halusinesheni za kusikia** hutokana na kusikia sauti zisizokuwepo
- **halusinesheni za mguso** hutokana na kuhisi kuwa umeguswa
- **halusinesheni za kuonjwa na kunusa** hutokana na kuonja kitu ambacho hujakula au kunusa kitu kisichokuwepo kama moshi



DELUSHENI NI NINI?

Delusheni ni mawazo au imani bila msingi wa ukweli. Mtu anayeugua PD hudhani kuwa mawazo haya ni ya ukweli. Kwa mfano, anaweza akadhani kuna mtu ambaye anataka kumfanyia mabaya, kumkimbiza au mpenzi wake sio mwaminifu. Delusheni huleta wasiwasi ikiwa vigumu kubainisha kama jambo ni la ukweli au la.



MBINU ZA KUPUNGUZA HALUSINESHENI AU DELUSHENI

- hakikisha kuna mwangaza wa kutosha jioni giza inapoingia
- mtu anapopata halusinesheni, kubaliana na yeye kuhusu mambo anayoona
- ikiwa halusinesheni hutokana na magonjwa ya kuambukizwa, kutibu magonjwa hayo humaliza halusinesheni hizo
- madawa mengine kama 'amantadine' yanaweza yakasababisha halusinesheni mionganoni mwa watu wazee
- wakati mwingine halusinesheni hutokana na shida ya usahaulifu, jambo ambalo linaweza likarekebishwa na madawa ya kutibu demenshia
- hakikisha unapata usingizi wa kutosha na jaribu kutolala mchana
- halusinesheni za kuona zinaweza zikatokana na shida za macho, hakikisha kuwa uwezo wako wa kuona unaangaliwa mara kwa mara
- ongea na familia yako kuhusu halusinesheni zako ili waelewe unachopitia

Jiunge na kikundi cha msaada
kilicho karibu ili ujifunze zaidi na
uonane na watu wengine waliyo na
ugonjwa wa parkinson

Kwa habari zaidi angalia:

Nairobi: 0722722090

www.parkinsonkenya.wixsite.com/website

Mombasa: 0707564733

AMA

Kisumu: 0710884431

www.parkinsonsafrica.com



Created by Natasha Fothergill-Misbah

